



**SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE  
OFFICE OF THE DEPUTY VICE-CHANCELLOR (ACADEMIC)  
P.O. BOX 3000 MOROGORO TANZANIA**

Tel.255-23-2603511/4, Dir:255-23-2603236 Fax:255-23-2604652  
Email: [dvc@suanet.ac.tz](mailto:dvc@suanet.ac.tz); [dvc.academic@yahoo.com](mailto:dvc.academic@yahoo.com)

**Our Ref: SUA/ADM/S.1/32**

**Your Ref:**

**Date: 22.07.2016**

Wanafunzi wote,  
Masomo ya Shahada za Awali (Undergraduate degree programmes),  
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,  
S.L.P. 3000,  
MOROGORO.

**RE: KUSOGEZWA MBELE MAFUNZO KWA VITENDO NA SUALA LA  
KUSAINI MIKOPO**

Tafadhali rejeeni kichwa cha habari hapo juu.

Kufuatia zoezi linaloendelea la kuhakiki wanafunzi wanufaika wa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo, Chuo kimeagizwa kusogeza mbele Mafunzo kwa Vitendo yaani "Field Practical and Teaching Practice Sessions" kwa kipindi cha wiki mbili kuanzia tarehe 25.07.2016. Hivyo basi kwa taarifa hii mnashauriwa kwenda nyumbani hadi Mafunzo ya Vitendo yatakapoanza rasmi kama serikali ilivyoelekeza.

Kwa vile kabla ya kulipwa fedha za mafunzo kwa vitendo mnatakiwa kusaini Fomu za Mikopo, imeamuliwa kwamba fedha za Mafunzo kwa Vitendo kwa wanafunzi wanufaika wa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo zitatumwa moja kwa moja kwa wanafunzi hao wakiwa nyumbani na Bodi ya Mikopo ili wanafunzi hao waweze kwenda kwenye maeneo husika na kuanza Mafunzo kwa Vitendo. Chuo kitatoa utaratibu ambao utatumika kusaini fomu za mikopo husika ili ziweze kurudishwa Bodi ya Mikopo.

Mnajulishwa zaidi kwamba iwapo kutakuwa na taarifa ya ziada kuhusiana na mabadiliko ya tarehe hizo mtajulishwa kadri tutakavyopokea maelekezo toka serikalini.

Wenu,

Prof. P.R. Gillah

**NAIBU MAKAMU WA MKUU WA CHUO (TAALUMA)**

- n.k. Makamu Mkuu wa Chuo      n.k. NMMC (Utawala na Fedha) } - Ndani ya Jalada.  
n.k. Msarifu  
n.k. Rais wa Serikali ya Wanafunzi